


# Mahekalu ni Nini?

Mahekalu ni majengo mazuri ambapo tunaweza kuhisi ukaribu na Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo. Kila hekalu lina maneno “Nyumba ya Mungu” yameandikwa juu yake. Hii hutukumbusha kwamba hekalu ni takatifu na tofauti na ulimwengu mwingine wote. Manabii wameahidi kwamba tunaweza kuhisi amani ndani ya hekalu.

- Hili ni hekalu la kwanza Thailand.
- Lina urefu wa ghorofa sita, pamoja na minara tisa.
- Wakati hekalu lilipokuwa likijengwa, dhoruba ilikaribia kuleta mafuriko. Lakini Roho Mtakatifu alimsaidia kiongozi wa mradi ajue kipi cha kufanya.



**Hekalu la Bangkok Thailand**

- Hili ni hekalu la pili lilijengwa Amerika ya Kati.
- Limetengenezwa kwa marumaru nzuri nyeupe kutoka Mexico.
- Hekalu liko umbali wa saa moja kwa gari kutoka kwenye volkano hai.



**Hekalu la San José Costa Rica**

Kata kadi, zikunje kwa kufuata mistari ya nukta na zigundishe zikiwa zimefungwa. Tafuta kadi zaidi za mahekalu kwenye [friend.ChurchofJesusChrist.org](http://friend.ChurchofJesusChrist.org)

